KITOVU CHA HUMAN RIGHTS DEFENDER HUB
TAARIFA YA SERA 3 | AGOSTI 2017



# Kuimarisha usalama wa mafunzo kwa watetezi wa haki za kibinadamu walio katika hatari

Ni nini watetezi wa haki za kibinadamu wanatia thamani kuhusu mafunzo ya usalama? Je, hii inaweza kufanywa vizuri? Je, mafunzo ya usalama yanachangia aje kulinda watetezi? Aina muhimu sana ya mafunzo si ile inayozingatia juu-chini, maarifa yakihamishwa kutoka wageni waalikwa, lakini ni yale: yanayo ongeza maarifa juu ya haki; kufanya uchambuzi wa mazingira, uchambuzi wa washikandau, na tathmini ya hatari; kutengeneza mazoea ya usimamizi wa usalama; kuongea na kushauriana; kujenga mitandao ya msaada; kutafakari juu ya matendo ya kila siku kuhusiana na usalama; na kupitisha ufahamu mbalimbali wa usalama unaojumuisha ustawi wa akili na kihisia.

## Utangulizi

Mafunzo ya usalama imekuwa njia muhimu ambayo watendaji wa ulinzi wanasaidia watetezi katika hatari ili waendeleze mazoea ya usimamizi wa usalama. Ikifanywa vizuri, watetezi walio katika hatari wanapata mafunzo yaliyo na thamani na wanataka zaidi. Walinzi watendaji hufanya mafunzo ya usalama kwa watetezi kwa njia tofauti, na mitindo tofauti ya utunzaji, na kwa ufafanuzi tofauti wa usalama. Sera hii ndogo inafupisha fikra na tafakari kutoka kwa watetezi zaidi ya mia nne walio katika hali ya hatari kutoka Colombia, Mexico, Misri, Kenya na Indonesia. Inaogelea juu ya mafunzo ya usalama, na kueleza yanavyoathiri wanachopendekeza kwa mafunzo ya usalama zaidi.

Katika utafiti huu, asilimia 64 kati ya washiriki 391 walisema kuwa wamepokea mafunzo rasmi juu ya jinsi ya kusimamia usalama wao wenyewe (tazama Jedwali 1). Asilimia 65 ya wanaume walipata wastani wa mafunzo 2.3 kila mmoja, asilimia 62 ya wanawake walipata wastani wa mafunzo 1.9 kila mmoja, na asilimia 60 ya watetezi wa transgender walipata wastani wa mafunzo 1.5 kila mmoja. Kwa ujumla, wanaume zaidi walipata mafunzo zaidi

kuliko wanawake. Hata hivyo, kwa sababu sampuli ya watetezi katika utafiti huu ni ndogo, asilimia ya watetezi walio hatarini katika kila nchi ambao wamepata mafunzo ina uwezekano kuwa chini sana.

Kuna njia nyingi ambazo mafunzo ya usalama hufanyika - kutoka kwa warsha zilizofanywa kwa wakati mmoja pekee (ambazo zinaweza kudumu siku kadhaa), kwa wale ambao wameingia katika uhusiano wa muda mrefu ambao wanaweza kujumuishwa ili kufuatilia hali yao mara kwa mara, kuambatana, kufundishwa, au kupokea msaada.

## Mkazo wa Mafunzo ya Usalama

*Ufahamu wa haki*

Watetezi katika utafiti wetu walithamini mafunzo ambayo yaliwasaidia kuendeleza ufahamu wao wa haki. Mafunzo ya usalama hupatia watetezi nafasi ya kujadili maana ya neno ' mlinzi wa haki za binadamu ' na haki ya kukuza na kulinda haki za binadamu kama ilivyoelezwa katika Azimio la mwaka wa 1998 juu ya haki na uwajibikaji wa watu, vikundi na viungo vya jamii kukuza na kulinda haki za binadamu na misingi ya uhuru kote ulimwenguni na vile zilivyolindwa na sheria za nchi.

*Uchambuzi wa mazingira ya nguvu, ya ndani*

Watetezi walithamini mafunzo ambayo yaliwawezesha kufanya uchambuzi wa mazingira kibinafsi na kwa pamoja kulingana na matokeo ya hivi karibuni, masuala ya sasa, na taarifa sahihi. Walibainisha umuhimu wa kupa kipaumbele matokeo yanayotokea katika ngazi za nchi. Walithamini fursa ya kujadili mambo na watendaji wanaopaswa kuhudhuria wakisimamia usalama wao binafsi katika mazingira yao maalum. Transwoman mlinzi kutoka Colombia alipendekeza kuwa "... mjadala zaidi unahitajika juu ya upekee, na mahitaji ya watu wanaohudhuria [mafunzo], kulingana na mazingira wanamoishi na kufanya kazi."

Watetezi walithamini kuzingatia utambuzi, uchambuzi na usimamizi wa vitisho na hatari kuhusiana na udhaifu wao na uwezo kama watu binafsi na kama makundi. Walisisitiza umuhimu wa kuchambua vitisho na mashambulizi yanayo wakumba kibinafsi. Kwa mfano, watetezi kutoka Colombia walibainisha umuhimu wa kuzingatia vitisho na watendaji wasiokuwa wa serikali, wakati watetezi kutoka Misri waliona haja ya kuchunguza vitisho kuhusiana na hali ya kisheria ya shirika lao na kukamatwa kwao na kushtakiwa.

Pia walisisitiza umuhimu wa kuwa na nafasi ya kutafakari juu ya hatari wanakabiliwa ambazo wanaweza kuwa wamepuuza katika maisha yao ya kila siku.

> *... ni kawaida kwa wanadamu ambao wanakabiliwa na hatari nyingi (wao wenyewe au wengine) kwamba inakuja wakati wamezoea kuongezeka kwa hatari, na kuanza kukataa haja ya usalama na mara kwa mara kujifunza kuhusu masuala. Hii inafanyika kwa watetezi wote.*
>
> **Mtetezi wa haki ya wafungwa wa kisiasa, kolombia**

Watetezi walibainisha umuhimu wa kuelewa hatari kuhusiana na miundo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, na usawa katika jamii, ambazo mara nyingi hazionekani. Mtetezi wa haki za wanawake na LGBTIQ * nchini Kenya alikosoa mafunzo ya usalama ambayo " ilipuuza muungano wa haki za kijamii na kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni ya jamii zetu".

Jedwali 1: Mafunzo ya Usalama iliyofanyika kwa Nchi

| Nchi | Je, umepokea mafunzo rasmi juu ya jinsi ya kusimamia usalama wako mwenyewe? | | | Wastani wa idadi ya mafunzo yaliyopokelewa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ndio | Hapana | Sina uhakika | Jumla | Wanaume | Wanawake | Transgender |
| kolombia | 68 % | 31 % | 1 % | 3.6 | 4.6 | 2.6 | 1.0 |
| Meksiko | 81 % | 16 % | 3 % | 2.8 | 3.1 | 2.6 | N/A |
| Kenya | 70 % | 29 % | 1 % | 1.7 | 1.9 | 1.5 | 1.0 |
| Indonesia | 59 % | 38 % | 3 % | 1.3 | 1.4 | 1.0 | 3.0 |
| Misri | 42 % | 46 % | 12 % | 1.0 | 0.7 | 1.4 | 1.0 |
| **Jumla** | **64 %** | **32 %** | **4 %** | **2.0** | **2.3** | **1.9** | **1.5** |



*[Mafundisho ya Usalama] ni muhimu lakini ni lazima iwe na uhusiano na kuwa muhimu kwa michakato ya kijamii nchini Mexico, kuangalia mbele ya hali ya sasa na kuzingatia hatari zilizopo, ambayo inaweza hata kuwezesha watu kuingilia harakati za kijamii au mashirika.*

**Mtetezi wa haki za kiraia na kisiasa, Meksiko**

Mafunzo ya Usalama husaidia watetezi kuongeza maarifa yao ya usalama na uangalifu wa kila siku. Kama mtetezi na mlinzi wa haki za wanawake nchini Kenya alivyona, "wamesaidia kubadilisha mtazamo wangu juu ya masuala ya usalama".

*Kujenga msaada wa kijamii na mitandao*

Mada yenye nguvu katika utafiti wetu ni jinsi msaada wa kijamii ulivyokuwa muhimu kwa usalama na ulinzi wa watetezi. Wakati wa shida, mara nyingi familia, marafiki, majirani, wanajamii na watetezi wenzake ndio ambao hutoa msaada wa haraka. Watetezi walielezea kwamba walitaka kujifunza zaidi kuhusu jinsi ya kujenga mitandao na vile itawasaidia kwa kazi yao.

Watetezi walisema jinsi migogoro,  na unyanyasaji katika harakati na mashirika ya haki za binadamu vina athari kubwa. Mtetezi wa haki za wanawake huko Mexico alisema hivi:

> *Wakati vurugu inatoka ndani, kutoka kwa wenzake wa karibu - kama washirika (wa karibu), wenzake kutoka kwa mashirika za utetezi, ndani ya harakati za kijamii - wakati hilo linatokea, kuna hatari ya kupasuka, wakati mwingine hata hatari zaidi kuliko yale yanayohusiana na watendaji wa nje ... tunahitaji kufanya kazi hiyo kwa mitandao ya watetezi ili kuwawezesha na kuwapa nguvu...*

Mwanasheria anayehusika na haki za ardhi kutoka Indonesia alithamini "usimamizi wa migogoro ndani na nje", na mlinzi kutoka Misri anayetetea haki za watetezi wa haki za binadamu alipokea "mwongozo na ushauri juu ya jinsi ya kukabiliana na migogoro na unyanyasaji".

*Mikakati na mbinu za kusimamia vipimo vingi vya usalama*

Watetezi walifurahia kujifunza njia za kujitetea. Walibainisha umuhimu wa kupata ujuzi wa usalama wa dijitali na teknolojia; kuzingatia usimamizi wa habari; kujifunza jinsi ya kulinda faragha wakati wa ufuatiliaji; na kujifunza jinsi ya kusimamia hatari zinazohusiana na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Watetezi walithamini mafunzo ya usalama ambayo yalitoa 'nafasi salama' ambako wangeweza kuzungumza juu ya uzoefu na hisia ambazo zilikuwa ngumu kushiriki. Mafunzo ya usalama yalikuwa fursa kwao kubadilishana mawazo juu ya jinsi ya kusimamia matatizo na hofu, na kujisikia kuthibitishwa na kuhimizwa. Kama kiongozi wa campesino kutoka Colombia alielezea, "Hatujiskii kuwa peke yetu kama hapo mbeleni". Kusisitiza juu ya kujitunza na ustawi wa kiakili na kihisia kulikuwa na thamani kubwa.

*[Mafunzo ya Usalama] ni muhimu kwa kila mtu katika shirika … [watetezi] wanapaswa kujua jinsi ya kuchukua na kupunguza hatari, kusimamia matatizo na hofu; kuelewa kwamba kazi yetu ni sababu inayohamasisha – tusitishwe na kushindwa na kampeni za kupakwa matope na vitisho, tuendelee kama timu moja na imara.*

**Mwanasheria anayefanya kazi kutetea haki za waathirika, Colombia**

Watetezi pia walibainisha umuhimu wa kutetea na kutegemea ulinzi na kinga ya taasisi.

## Mazingatio ya ufundishaji

Thamani zaidi ya mafunzo ya usalama ni ile hasa inayolingana na mahitaji maalum na mazingira ya watetezi. Watetezi walibainisha kuwa hatari zinatofautiana kutoka sehemu moja ya kijiografia hadi nyingine. Mlinzi kutoka Mexico anayefanya kazi kwa haki za kiraia na za kisiasa alinena,

> *Warsha mara kwa mara hazilengi masuala maalum. Mexico ukweli ni kuwa hali ni ngumu na inachanganya na pia inabadilika haraka sana. Ukilinganisha na vile nchi ilivyokuwa miaka kumi imeipita, kila jiji au idadi ya watu imebadilika hubadilishana kwa kasi.*

Watetezi walithamini mafunzo ya usalama yaliyotengenezwa baada ya wao kushauriwa, na kutolewa kwa lugha yao wenyewe, kwa kutumia mbinu za mafunzo zinazofaa kwao.

Mara kwa mara, watetezi walisema kwamba walitaka mafunzo ambayo ilikuwa ya kimkakati na ya vitendo, sio tu ya kinadharia. Walithamini mapendekezo halisi yaliyotumika katika maisha ya kila siku kutokana na hali zao na vikwazo. Wengine pia waliona kwamba hawakuweza kutekeleza kila hatua ambazo zilipendekezwa na walimu wao.

*[Ni muhimu] kutoa njia ambazo ni rahisi kupata; kuendeleza maisha ya siku kwa siku. Mapendekezo mazuri zaidi, majadiliano mafupi. Itakuwa bora kutoa mifano tatu tu halisi ya mambo ambayo yanaweza kufanywa. Mazoezi na [jina la shirika] lilikuwa la kustua sana kwani kwa mapendekezo yao, walikuwa wanatia chumvi sana. Walitoa mapendekezo mengi ya kuchukua wakati wa tahadhari mtu hawezi kukumbuka yote. Walitupa mengi sana kila mtu alitoka mafunzo hayo akihisi wasiwasi.*

**Mwanasheria anayefanya kazi kwa haki za waathirika, Colombia**

Watetezi walitaka kupata mafunzo ya kawaida zaidi. Kama mlinzi kutoka Mexico alivyosema, "Ni muhimu lakini hazitoshi na kwa kawaida wadhamini hawafuatilii vile tunavyo endelea. " Walisema pia ni muhimu kwa mafunzo kufanyika kwa watetezi zaidi, ikiwa ni pamoja na wanachama wa jamii (sio viongozi), watetezi katika maeneo ya vijijini, na watetezi wa wanawake.

Watetezi hawakupenda mafunzo ambayo yanayofanywa kwa haraka kwani hayatoshi. Hawakupenda mafunzo ambayo wakufunzi hawajui mazingira ya ndani vizuri, kama vile mwanasheria anayefanya kazi ya madini na haki za mazingira nchini Kolombia aliona, "ni kama kutazama nje wa hali … kutoa maamuzi kwa mbali" . Kiongozi wa Afro-Colombia alielezea umuhimu wa kuwa na "ushirikiano wa watu wanaozungumza kwa maneno yao wenyewe, akielezea yaliyotokea kwao, ili kuwasilisha ndani ya jamii". Mtetezi mwingine kutoka Colombia anayefanya kazi kwa haki za watu wa LGBTIQ * alisema,

> *Wanahitaji kuwa na ushirikishi zaidi pamoja na ujuzi wa watu wa ndani na watu walio katika hatari zaidi. Wanahitaji kuonyesha maoni ya watu ambao wana uzoefu zaidi, ambao, bila shaka, ni watu walio katika hatari na watu katika maeneo mbali mbali. Kuna haja ya kuwa na mazungumzo zaidi na wao.*

*Watu ambao wameishi migogoro yenyewe kibinafsi ni bora wawe wakitoa warsha kwa sababu wakufunzi wengine mara nyingi hawaelewi mazingira. Nadhani kuwa na mtazamo mara mbili inaweza kuwa ya kweli ya kuvutia. Kwa mfano, kulinganisha kati ya nchi zilizo na au hali hiyo inaweza kutufundisha mengi. Kwa mfano, kulinganisha kati ya hali ya madini katika Guatemala na hali ya madini huko Colombia.*

**Mwanamke mlinzi anayehusika na haki za madini na mazingira, Colombia**

Baadhi ya watetezi walibainisha thamani ya kutumia mfano wa majukumu ya kazi katika warsha ili kuwasaidia kutarajia matukio, vitisho, na kukabiliana na hatari kwa njia za vitendo. Pia walipenda kutumia masomo ya kesi kulingana na matukio halisi na uzoefu. Walifurahia mbinu za mafunzo ambazo zilihusisha ushirikishwaji wa kazi na ambazo zilikuwa zikizingatia mahitaji yao na wasiwasi wao.

Watetezi walithamini nafasi za kushiriki uzoefu wao binafsi na kuuliza maswali. Kama mtetezi kutoka Colombia akifanya kazi ya kutetea haki za watu wa LGBTIQ *

> *[Mafunzo] ni mafupi sana. Mara nyingi, wakufunzi huingia kwenye ndege hiyo asubuhi, na kuondoka kwa ndege mchana huo huo. Watu (HRD na watu walio katika hatari) wanataka kuongea juu ya matukio yao na mkufunzi. Wanapata msisimko sana kuzungumza nao na kuzungumza juu ya uzoefu wao. Kuna haja ya kuwa na muda wa kuzungumza juu ya uzoefu wao na kisha kuuliza maswali.*

Watetezi walifahamu wakati chakula, usafiri na malazi kuhusiana na mafunzo zililipwa na wadhamini.

Watetezi kadhaa walipendekeza kuwa itakuwa manufaa kuhusisha watendaji wa serikali katika mafunzo ya usalama. Kama kiongozi wa haki za wanawake wa campesino kutoka Colombia alivyosema,

> *Huzisha mamlaka za serikali zinazohusika na ulinzi wa watetezi kwa njia inayowafanya wahisi kwamba wanapaswa kutekeleza mipango yao ya kazi na kuwajibika kikamilifu kwa dhamana za kutetea na kutetewa dhidi ya ukuikaji wa haki za kibinadamu.*

Hata hivyo, baadhi ya watetezi waliogopa sana njia hii, kwa sababu inaweza kuharibu uaminifu unaohitajika kwa ajili ya mafunzo ya usalama. Pia, walihofia kuwa maafisa wa serikali wanaweza kuonekana kuwa na wasiwasi juu ya ulinzi wao bila sababu yoyote.

Watetezi walibainisha thamani ya wakufunzi wa kutoka nje, lakini pia kwamba walipaswa kuweka ujuzi na kujifakari kwa mafundisho yao. Kama mlinzi kutoka Colombia alielezea, kile kilichohitajika kutoka nje kilikuwa 'kidogo, cha kusaidia; mengi imo ndani ya kubadilisha '.

## Vidokezi kwa utendaji

- Kutambua kwamba mafunzo ya usalama ambayo inatofautiana na hali ya kila siku ya watetezi, mara nyingi hayana ufanisi. Watetezi wenyewe wanapaswa kupata mafunzo ya usalama na msaada wao kuwa wa manufaa.
- Kusaidia watetezi (watu binafsi, makundi, jamii, na mashirika) katika kuunganisha masuala ya usalama na usimamizi katika maisha yao ya kila siku. Tambua kuwa kwa makundi, mienendo ya vikundi vinaathiri tabia, na mazoea ya kila siku.
- Saidia kutoa mafunzo ya usalama ambayo yanafaa kwa mazingira maalum na mahitaji ya watetezi katika hatari. Shirikisha watetezi katika mipango ya mafunzo na kupata mitazamo yao.
- Kuhakikisha kwamba mafundisho yamewafikia watetezi ambao sio rahisi kuwafikia (hasa wale walio katika maeneo ya vijijini); watetezi wa wanawake; watetezi wa haki za LGBTIQ; na watetezi wa haki za ardhi na mazingira.
- Tenga nafasi wakati wa mafunzo ya usalama ambapo watetezi wanaweza kuzugumza juu ya jitihada zao, na hisia, lakini ikilinda dhidi ya unyanyasaji tena.
- Saidia watetezi katika kuendeleza na kutekeleza mipango ya utekelezaji wa usalama wao ambayo inayowezekana, na inayoweza kutolewa kutokana na hali halisi na vikwazo. Kuwasaidia kutambua msaada wanaohitaji kwa utekelezaji wa mipango kama hiyo na kuwasaidia kuijenga.
- Wasaidie watetezi katika kujenga mitandao na msaada kwa kazi zao katika ngazi mbalimbali. Kuwezesha kutafakari binafsi juu ya sababu za migogoro ndani ya wanaharakati na mashirika ya haki za binadamu na jinsi hizi zinaweza kusimamiwa. Kuhimiza kutafakari jinsi unyanyasaji na unyanyasaji wa kisiasa vinavyochangia kwenye migogoro ya kibinafsi na mvutano.
- Kuunganisha mafunzo ya usalama na hatua nyingine za kuimarisha usalama wa watetezi, kama vile msaada wa dharura katika hali ya hatari na maendeleo ya muda mrefu ya mazingira ya kuwezesha kulinda na kulinda haki za binadamu.

**Kuhusu Mradi huu:**
Taarifa ya Sera hii inatokana na matokeo ya utafiti ya mradi 'Kuepuka Hatari, Kumudu Usalama, na Kupokea Msaada' ambao unachunguza uzoefu wa watetezi wa haki za binadamu waliomo hatarini Kolombia, Meksiko, Misri, Kenya, na Indonesia.

Mahojiano na tafiti zilifanyika na zaidi ya watetezi wa haki za binadamu 400 kati ya Julai 2015 na Novemba 2016.

UNIVERSITY of York

Centre for Applied Human Rights
University of York
Yorkshire House
6 Innovation Close, York Science Park
Heslington, York YO10 5ZF
United Kingdom

+44 (0)1904 325830
cahr-admin@york.ac.uk
***york.ac.uk/cahr***

**Mtafiti Mkuu:**
Alice M. Nah

**Research Team**
Sherif Azer
Patricia Bartley
Peter Cousins
Indria Fernida
Kholoud Hafez
Budi Hernawan
Irina Ichim
Katrina Maliamauv
Erick Monterrosas
Patrick Mutahi
Paola Pacheco Ruiz
Emily Schmitz

**Kwa taarifa Zaidi:**
***securityofdefendersproject.org***
security-of-defenders-project@york.ac.uk

**Marejeo**
Nah, A.M. (2017) Strengthening Security Training for Defenders at Risk, Human Rights Defender Hub Policy Brief 3, Centre for Applied Human Rights, University of York: York, available at ***securityofdefendersproject.org***

**Mchoraji**
Lara Luna Bartley

**Kubuni**
Design and Print Solutions

37735 – york.ac.uk/design-print-solutions